

Croup (Swahili)

Kifaduro



Kifaduro ni ugonjwa wa kupumua unaosababishwa na virusi. Virusi hivyo husababisha zoloto (sanduku la sauti), trakea (koo ya pumzi) na bronki (njia kubwa ya hewa kwenye mapafu) kuvimba ambako hufanya iwe vigumu kwa mtoto wako kupumua. Watoto walio na kifaduro huwa na kikohozi kikali na kubweka na wanaweza kutoa sauti yenye kilele ya juu wanapovuta pumzi.

Kifaduro huathiri zaidi watoto kati ya miezi 6 na miaka 6 lakini inaweza kuathiri watoto wakubwa. Ni kawaida zaidi katika msimu wa baridi.

Ishara na dalili

Kifaduro kawaida huanza na siku 1 au 2 za dalili za kawaida za baridi (homa ndogo na pua yenye makamasi). Kama virusi inapoenea mtoto wako anaweza kupata:



kikohozi cha kubweka (kinaweza kusikika kama sili)
sauti nzito



sauti za kelele wakati wa kuvuta pumzi
shida ya kupumua
kupumua kwa kasi kuliko kawaida
koo ya kuumia



kupoteza hamu ya kula (pamoja na kutotaka kunywa)

Mara nyingi dalili huanza ghafla usiku na zinaweza kuwa bora wakati wa mchana.

Matibabu

Kwa kawaida watoto hujisikia vizuri ndani ya siku 3 hadi 4 bila matibabu yoyote. Daktari anaweza kupendekeza yafuatayo ili kusaidia na dalili:

- dawa za maumivu kama vile paracetamol (Panadol au Dymadon) au ibuprofen (Nurofen)
- dawa ya kioevu (steroidi) kwa kupumua kwa kelele kwa mtoto wako. Hii inaweza kupunguza kupumua kwa kelele kwa mtoto wako ndani ya saa chache, lakini kikohozi chake kinaweza kuendelea hadi wiki 2.
- dawa kwa njia ya maski (nebulizer) kwa dalili kali.



Utunzaji wa nyumbani

Kesi nyingi za kifaduro zinaweza kutibiwa nyumbani kwa usalama. Unaweza kumsaidia mtoto wako kujisikia vizuri zaidi kwa:

- kumfanya mtoto wako kuwa mtulivu (kilio kinaweza kufanya sauti ya kifaduro iwe mbaya zaidi)
- kuhimiza mtoto wako kukaa wima (hii inaweza kumsaidia kupumua kwa urahisi)
- kumpa dawa ya kutuliza maumivu kama paracetamol au ibuprofen. Fuata maelekezo kwenye chupa au paketi kwa kipimo cha sahihi. Usimpe mtoto wako kipimo zaidi ya kile kinachopendekezwa kwa siku.

Kwa ushauri wa matibabu usio wa dharura, piga simu 13 HEALTH (13 43 25 84) kuzungumza na muuguzi aliyesajiliwa saa 24 kwa siku, siku saba kwa wiki kwa gharama ya simu ya mtaa.



Omba kupata mkalimani ikiwa unamhitaji.

Wakati wa kuonana na daktari

Mwona daktari wako ikiwa mtoto wako ana dalili za kifaduro. Daktari atamchunguza mtoto wako na kuuliza kuhusu dalili zake na kama amekuwa akiugua kifaduro hapo awali. Vipimo havihitajiki kwa kawaida.

Mpeleke mtoto wako kwa idara ya dharura iliyo karibu ikiwa amegunduliwa na kifaduro na hali yake inazidi kuwa mbaya.

Piga simu kwenye Sifuri Mara Tatu (000) mara moja ikiwa mtoto wako:

- anapumua haraka sana
- anatatiza ya kupumua
- ni rangi ya mweupe, bluu au kijivu.

Imeandaliwa na Idara ya Dharura, Hospitali ya Watoto ya Queensland. Tunatambua mchango wa watumiaji na walezi.

Resource ID: FS011 **Reviewed:** July 2022

Kanusho: Maelezo haya yametolewa na wataalamu wa afya kama mwongozo pekee na yanalenga kusaidia, si kubadili nafasi, majadiliano na daktari wa mtoto wako au wataalamu wa afya. Taarifa husasishwa kila mara, kwa hivyo tafadhali angalia kuwa unarejelea toleo la hivi majuzi zaidi. Tafuta ushauri wa matibabu, inapofaa, kwa wasiwasi kuhusu afya ya mtoto wako.